# *Ukombozi Kwa Nguvu*

Asanteni, sana. Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kuwa hapa usiku wa leo, kuwanenea tena katika Jina la Bwana wetu mpendwa Yesu Kristo. Na daima ni majaliwa kukutana na watu wa Mungu, popote, na kunena juu ya Jina hilo kuu, Yesu.

2 Hakika nauthamini wimbo ambao ndio kwanza ndugu yetu auimbe. Huo, huo ndio ninaoupenda zaidi. Katika siku ambayo wanajaribu kumfanya Yesu kuwa nabii tu, au mtu mwema, au mwalimu, huo kwa kweli huleta Uungu Wake, kile Yeye alichokuwa. Nami naamini ya kwamba alikuwa . . .

3 Kamwe hapajakuwa na Mmoja kama Yeye, duniani, hatakuwepo. Alikuwa Imanueli. Yeye alikuwa Alfa, Omega; mwanzo na mwisho; Yeye aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja; Shina na Mzao wa Daudi; Nyota ya Asubuhi. Ndani Yake ulikaa Uungu. Ndani Yake alikuwamo Mungu.

4 "Mungu alikuwa ndani ya Mwanawe, ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Yesu alisema, "Si Mimi nizifanyaye kazi hizo, bali ni Baba Yangu aishiye ndani Yangu. Mimi na Baba yangu tu mmoja," Mungu akidhihirishwa, katika mwili. Ni ufunuo wa ajabu jinsi gani wa upendo wa Mungu kwetu, angejifunua Mwenyewe na kushuka na kukaa katika mwili wa mwanadamu, ili kuondoa dhambi na magonjwa kutoka kwa wanadamu, na kutukomboa turudi kwa Baba. Hiyo ni ya ajabu, sivyo? Hakika tunathamini jambo hilo.

5 Sasa, jana usiku, nafikiri itanibidi kwa namna fulani kuomba msamaha. Mimi . . . Billy alinipata, upesi kidogo, jana usiku, kwa maana ilikuwa kwa namna fulani . . . Nikawa dhaifu. Lakini mikutano hiyo, upambanuzi huo, na hakuna mtu atakayejua kamwe hiyo ni nini, isipokuwa ni ninii tu . . . Huna budi kuingia ndani yake, ili kujua jambo hilo, unaona. Hakuna njia ya kujaribu kuielezea. Hakuna nji—njia ambayo unaweza kuifanya. Ni uzoefu tu kwamba—kwamba hakuna anayejua habari zake, ni wale tu wanaoupitia. Kile unachofanya kwa jamii ya wanadamu, kile unachofanya kwa mwanadamu, huleta uhai ule ule kutoka kwake!

6 Vema, unaishi katika ulimwengu mbili. Uko katika ulimwengu *hapa,* na uko katika ulimwengu *kule,* ukiwa na mtu mwingine, labda miaka hamsini iliyopita; na unaweza kuwa na mtu fulani, miaka kadha kuanzia leo, ijayo; na bado unatambua kuwa umesimama kwenye jukwaa hapa, na unazungumza jambo lililotokea miaka mingi, mingi iliyopita; labda majuma kadha yaliyopita, miezi kadha iliyopita; taifa lingine, mahali pengine, ama chochote kile. Na kisha unajaribu kujiweka sawa, katika hilo, na kuwazia; nakwambia, ni jambo kubwa mno. Lakini

Bwana ametubariki hadi sasa, ndani yake, nasi tuna furaha sana, na tunatumaini sasa ya kwamba Mungu atapata utukufu kutoka kwenye mkutano.

7 Sasa, katika i—ibada za usiku wa leo, niliwazia, wakati tuko watu wachache tu, pamoja; mikutano yetu inatangazwa tu hapa nyumbani, na ni ya wenyeji tu. Na kabla hatujaingia katika sehemu kubwa ya mikutano, nilikuwa nikiwazia, leo, ya kwamba ningejaribu labda kupata baadhi ya mafundisho ya mtindo wa kale, kutoka katika Biblia, kwa watu; kwamba wakati tukio kuu likija, kama Mungu atalituma kwetu, basi tutaweza kulielewa vyema zaidi.

8 Baada ya yote, uponyaji wa Kiungu ni cha—chambo tu kwenye ndoana, ili kukamata samaki, kama unavyojua. Ni kwamba tu hiyo ndiyo. . .Samaki hushika chambo na kupata ndoano. Kwa hivyo ninii yetu kuu. . .Mwisho wetu mmoja ni huu, kwamba, nafsi zimeletwa kwa Yesu Kristo.

9 Mungu akikuponya usiku wa leo, unaweza kuugua tena kabla hujafa. Unaweza kuwa mgonjwa tena, katika mwaka mmoja kutoka sasa, au miaka miwili kutoka sasa; unaweza kuwa mgonjwa baada ya wiki moja kutoka sasa, au siku moja kutoka sasa. Sijui. Lakini kuna jambo moja hakika, utaondoka katika ulimwengu huu, baadhi ya siku hizi, maana hii imetiwa kiraka tu.

10 Lakini nafsi hiyo ikiwahi kugusana na Roho Mtakatifu na kuzaliwa mara ya pili, una Uzima wa Milele. Haijalishi nini kitatokea hapa, hutaangamia kamwe. Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, anao," hiyo ni wakati uliopo, "Uzima wa milele, hataingia katika hukumu; bali amepita," wakati uliopita, "amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Hilo lingetufanya sisi sote Wamethodisti na tuanze kupaza sauti, (sivyo?) hiyo ni kweli, kuwazia jambo hilo, ya kwamba Mungu amefanya jambo hilo. Sasa, hilo si neno langu; hilo ni Lake, Yohana Mtakatifu 5:24.

11 Yohana Mtakatifu 6, Yesu alisema, "Aulaye mwili Wangu, na kunywa Damu Yangu, yuna Uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho." Hiyo ni kweli. "Aulaye mwili Wangu, na kunywa damu Yangu, yuna," hiyo ni wakati uliopo, "Uzima wa milele." Sasa, hii "milele," haitoki tu kutoka kwa uamsho mmoja hadi mwingine, bali inapitia Umilele.

12 Na sasa, kwa baadhi yenu wahudumu ambao mmeketi karibu, tukijua kuwa huo "Uzima" wa milele linatokana na neno lile lile linalomaanisha "Uhai wa Mungu." Neno Zoe, neno la Kiyunani, ambalo linamaanisha "Uhai wa Mungu Mwenyewe."

13 Kisha, tunakuwa mwana ama binti wa Mungu, mzao wa Mungu, tukiwa na sehemu ya Uhai wa Mungu ndani yetu. Hatungeweza kuangamia zaidi ya vile Mungu angeweza kuangamia, kama ingejaribu. Kwa hiyo, tuna Uzima wa

milele; na tutafufuliwa katika siku ya mwisho. Ajabu hiyo? Hilo lingewafanya Wabaptisti, Wamethodisti, kusalimiana kwa mikono na kupaza sauti. Sivyo? Hakika lingefanya. Hiyo ni kweli.

14 Hilo ndilo jambo jema kuhusu dini ya mtindo wa kale. Inafanya tu kila mtu kukaa pamoja na kupendana. Hakika inafanya. Huondoa tofauti zote, hufanya viumbe vipya. Itafanya ko—koti rasmi, na jozi ya ovaroli, kukumbatiana na kusema, "Ndugu, unaendeleaje?" Hiyo ni kweli. Hakika itafanya. Itafanya vazi la hariri, na kaniki, kukumbatiana na kusema, "Dada, nakupenda." Hivyo ndivyo ifanyavyo. Hakika hufanya hivyo, inabomoa tu tofauti. "Tajiri au maskini, mtumwa au huru, sisi sote tu kitu kimoja katika Kristo Yesu."

15 Jumapili, kwenye maskani, ambayo ninaona kuna kundi zima la watu wa maskani wanaoketi hapa, tulikuwa na—tulikuwa na so—somo la shule ya Jumapili, "ukombozi kwa damu." Nami nilijisokota sana ndani yake, hata ninahisi kama ningali katika nyanja nyingine mahali fulani, kwenye: *Ukombozi Kwa Damu*.

16 Na usiku wa leo, baada ya familia kuondoka na kuja hapa mapema, kupata kusikia ibada ya nyimbo, na kadhalika, nilikuwa chumbani. Na ilionekana kama . . . Nikaanza kusoma katika Maandiko, na nikapata kitu. Nikawazia, "Vema, Bwana akipenda, nitazungumza tu juu ya hilo kwa muda kidogo usiku wa leo."

17 Hiyo ni, *Ukombozi Kwa Damu,* Jumapili. Sasa, usiku wa leo, nitazungumza juu ya *Ukombozi Kwa Nguvu*. Na kesho usiku nitazungumza juu ya *Ukombozi Katika Utimilifu,* (Mungu akipenda, yaani), *Katika Furaha*. Katika damu, katika nguvu, na katika furaha; ukombozi!

18 Na kuvuta hii . . . Sasa, watu wengi, kama ambavyo wasomi mashuhuri, wenye elimu wanavyojua jinsi ya kupenya na kutoa ufunuo wa namna hii, labda, kwa ajili ya *hili,* ama *lile,* ama kutupa mengine. Lakini, mimi, kwa namna fulani mimi ni mmoja wa hawa wahubiri hapa wasio na elimu ambao . . . Kitu pekee ninachojua kufanya, kuwa na hakika ya kwamba niko karibu sana kuwa sahihi, hata hivyo, ni kwenda kwenye vivuli. Kama ningeanza kuelekea ukutani, na nuru upande *huu*, ningeweza kusema ni nini, karibu tu jinsi nilivyoonekana; kama nilikuwa mnyama mwenye miguu minne, ama—ama ndege, ama chochote kilichokuwa, nikiona ni aina gani ya kivuli ninachoakisi.

19 Sasa, Agano la Kale lilikuwa ni kivuli cha Agano Jipya. Ilikuwa ni negativu. Kama mwezi, kwa jua; jua linapoangaza juu ya mwezi, huangazia nuru dunia. Na ninapenda tu Agano la Kale! Limejaa mafumbo namna hiyo, ama, liwezavyo kuwa. Sasa, ninii kamili . . .

20 Katika Mwanzo, wakati Mungu aliumba ju—jua, kwanza, halafu mwezi ukafuata, mwezi na jua vinawakilisha Kristo na Kanisa. Kama vile tu jua huchomoza katika nguvu na utukufu wake; na linaposhuka, huangazia nuru yake kwa mwezi, gizani, kutoa nuru juu ya dunia wakati jua limetua. Yesu, alipoondoka, aliingia Utukufuni na kuakisi Nuru Yake juu ya Kanisa; kutoa, Kanisa, Nuru ya Injili mpaka atakaporudi, loo, jamani, ndipo watafunga ndoa. Hiyo itakuwa ya ajabu. Itakuwa Nuru moja kuu ya mwezi na . . . "Mwanakondoo ndiye nuru yake." Hawakuhitaji jua tena, katika Mji huo.

21 Sasa kwa utangulizi kidogo, hebu turejee kwenye Kutoka. Na ninatumai hamtachoka nami kuzungumza katika Kutoka.

22 Wakati mmoja, katika kanisa langu ng'ambo ya mto, nilihubiri, naamini, yapata mwaka mmoja na miezi sita, juu ya Ayubu, kila usiku. Wangerudi; ningechukua tu sehemu ndogo ya Ayubu, na, tukiendelea, tungeipitisha kote katika Biblia.

23 Kila Andiko linafungamana pamoja. Hakuna kuhitilafiana katika Neno la Mungu. La, bwana. Kila chembe, kamilifu! Kitabu pekee kilichowahi kuandikwa ambacho kimevuviwa namna hiyo, ambacho kinaweza kikamilifu . . . Kilichoandikwa na waandishi wengi, na mamia mengi mbalimbali ya miaka; na kila mmoja wao, kwa Roho Mtakatifu akinena, yanaingiliana moja kwa moja. Hiyo ndiyo sababu, kwenye vitabu hivi vyote vya ziada, Makabayo na kadhalika, haipatani na Hili, kwa hiyo sivikubali. *Hili ni* Neno la Mungu, kwangu mimi.

24 Na mwanamke fulani aliniandikia barua na kusema . . . Nilikuwa nikihubiri; Ayubu kwenye lundo la majivu. Akasema, "Ndugu Branham, umekuwa, na Ayubu kwenye lundo la majivu yapata muda wa kutosha, sivyo? Umekuwa hapo kama wiki sita." Kasema, "Mbona, hivi utawahi kumtoa kwenye lundo la majivu?"

25 Vema, nikasema, "Wakati Roho Mtakatifu atakapoacha kuyasukuma Maneno kutoka hapo, nafikiri itabidi niache kulisema." Lakini mradi alinifanya nizungumze juu yake kwenye lundo la majivu, vema, nilidumu tu nalo moja kwa moja; na nafsi zikiokolewa.

26 Kwa hiyo, kama mwinjilisti, alikuja mjini. Alihubiri, usiku mmoja, alihubiri juu ya toba. Usiku uliofuata, akahubiri juu ya toba. Usiku uliofuata, akahubiri juu ya toba. Baada ya kama siku nne ama tano usiku, baraza la mashemasi lilikutana naye na kusema, "Ndugu, huwezi kuhubiri kitu kingine chochote zaidi ya toba?"

27 Kasema, "Loo, naam. Hebu wote watubu, kwanza, ndipo nitahubiri juu ya jambo lingine." Kwa hivyo hilo ni wa—wazo zuri. Wao, kila mmoja, atubu, ndipo tunaweza kuhubiri juu ya jambo lingine. Vema.

28 Kwa utangulizi kidogo sasa, kwa wale, ama hasa wale ambao hawakuwa kwenye Maskani Jumapili asubuhi. Tunataka kurudi kwenye sura ya 12. Lakini wazo letu la msingi usiku wa leo liko katika mlango wa 14, kuanzia kifungu cha 13 cha Kutoka. Sasa, tuliachia kwenye kifungu cha 10, Jumapili asubuhi, ya *“ukombozi kwa damu.”* Wengi wenu mnaifahamu hadithi hiyo, nina hakika.

29 Sasa tunajua ya kwamba tungeweza kuvuta nyuma karatasi za Kitabu hiki, na kugeuza kurasa hizi. Lakini kuna Mmoja tu Ambaye anaweza kukifungua kile Kitabu, huyo ni Yesu Kristo.

30 Yohana alikiona Kitabu hicho. Kilikuwa kimefungwa kwa mihuri. “Naye akalia kwa sababu hapakuwa na mtu Mbinguni aliyeweza kukifungua, hakuna mtu duniani, hakuna mtu chini ya ardhi. Lakini kulikuwako na Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, akaja akakitwaa Kitabu katika mkono wa kuume wa Yeye aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi, akaifungua mihuri na—na kufungua Ki—Kitabu, akaifungua mihuri yake. Naye alistahili, kwa maana alikuwa amechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

31 Hebu tuzungumze Naye, usiku wa leo, na kumwomba Yeye atufungulie sasa hivi.

32 Sasa, Baba mwenye fadhili, mwenye upendo, tunakuja Kwako, tukizungumza Nawe, kwanza, katika Jina la Yesu. Tukiomba sasa, ya kwamba, tunaposimama hapa, tukiwa tumejificha chini ya paa hili, usiku wa leo, ambapo dhoruba hiyo inavuma nje, mvua ikipinda na kuvuma, tunashukuru sana kuwa na nyumba ya Mungu ya kuingia ndani. Na tunashukuru kwamba kuna mnara, kimbilio; Ulisema, “Jina la Bwana ni ngome imara; wenye haki huikimbilia wakawa salama.” Tuna furaha sana kwamba tunajua Jina la Bwana, na tumeingia ndani Yake.

33 Sasa tunaomba ya kwamba utatufungulia Neno hili, usiku wa leo, Baba. Jalia Roho Mtakatifu aje na kuingia kwenye Neno. Itahiri midomo ya maskini mtumishi huyu mnyenyekevu, na mioyo ya wale watakaosikiliza, watoto Wako. Na jalia Roho Mtakatifu achukue tu Maneno ya Mungu na kuyaweka katika kila moyo, pale tu yanapohitajika. Utubariki sasa. Fanya upya nia zetu, usiku wa leo, katika Roho Wako. Pata utukufu kutokana na ibada hii. Waokoe waliopotea. Waponye wagonjwa. Warudishe Nyumbani waliorudi nyuma, Bwana. Nasi tutakupa sifa, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lako, la Mwanao mpendwa, Yesu. Amina.

34 Sasa fungua kifungu cha 10 cha mlango wa 12 wa Kutoka. Tulikuwa tunasoma, *“ukombozi kwa damu,”* jinsi ambavyo Mungu alikuwa ameagiza mwana-kondoo achinjwe katika kila nyumba, jinsi ambavyo kulipaswa kusiwe chochote kilichobakishwa.

35 Hukumu zilikuwa zikianguka, na hukumu ya mwisho sasa ilikuwa tayari kuanguka. Mungu alikuwa anaenda kutimiza Neno Lake, kikamilifu. Na hukumu hizo zote kule nyuma zilikuwa ni ishara kamilifu, ama mfano mkamilifu, wa hukumu ambazo ziko tayari kuanguka sasa.

36 Na kama utatambua, kabla hukumu haijaanguka. Sasa wahudumu wanaweza kutokubaliana nami juu ya hili, jambo ambalo ni sawa. Lakini kabla hukumu haijaanza kuikumba Misri, Mungu aliwatuma Israeli kwenda Gosheni. Walikuwa Gosheni, na hakuna tauni iliyowapata. Mfano mkamilifu wa Kanisa lililobebwa, kupitia ile dhiki, unaona. Vema.

37 Ndipo katika pigo la mwisho lililoipiga nchi pale, ama kuipiga Misri, lilikuwa ni mauti. Ninyi nyote wasomaji wa Biblia hapa, mnajua masomo yenu ya shule ya Jumapili na kadhalika, mmechukua hili, pengine, mara nyingi. Lakini, kifo kilikuwa adui wa mwisho aliyeipiga Misri.

38 Na adui wa mwisho ambaye atalipiga kanisa sasa ni mauti, tukinena kiroho. Wale ambao hawatamfuata Kristo, katika—katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, watakauka kiroho na kufa; makanisa, mnaweza kuyaona sasa. Baada ya miamsho mingi, mingi mikubwa na wainjilisti kupita katika nchi, na, hata hivyo, kanisa, yaani, kusema kanisa-kisiasa, linazidi kuwa baya kila wakati. Washiriki wake wanaishi tu jinsi wanavyotaka, wanafanya chochote wanachotaka, hata hivyo, wakijiita Wakristo, na kusema wako sawa.

39 Kuwa *Mkristo,* maana yake ni kuwa "kama Kristo." Usiende mahali popote ambapo hungependa kuwapo kama Kristo angekuja. Usiseme chochote ambacho hungependa kusema wakati Kristo atakapokuja. Usifanye chochote ambacho hungependa kufanya wakati Kristo atakapokuja. Usiwazie chochote ambacho hungependa kuwaza wakati Kristo atakapokuja. Dumisha nia yako moja, moyo wako ukizingatia Kalvari. Amina. "Enendeni katika Nuru, kama Yeye alivyo katika Nuru, nasi tuna ushirika sisi kwa sisi, na Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, hutusafisha na uovu wote." Hao ni Wamethodisti, Wabaptisti, na sisi sote, pamoja, hutufanya sisi sote kuwa kitu kimoja ndani Yake.

40 Sasa, jambo la mwisho, jambo la mwisho lilikuwa kifo. Na kabla ya kifo hicho kuja, kulikuwa na upatanisho uliofanywa kwa ajili ya kifo hicho, kwa ajili ya wote wanaotamani kukiepuka.

41 Na kulikuwa na upatanisho uliofanywa kabla ya uharibifu wa kwanza, wa ulimwengu uliotangulia gharika. Mungu alikuwa na mhubiri wa haki, Nuhu, naye alihubiri miaka mia moja na ishirini, ili watu waingie katika safina. Na wale ambao walikataa makusudi kwenda, hapakuwa na chochote kilichosalia ila hukumu.

42 Na, leo, mtu anayekataa kutembea katika Nuru ya Kristo, umeikataa rehema, kwa hiyo hakuna kilichosalia ila hukumu. Ni hayo tu. Kuna tu upande wa kulia na wa kushoto, moja tu unaweza kwenda. Na unafanya chaguo lako.

43 Sasa, tunaona, kabla ya ule—ule usiku wa kutisha kuja, ambao Israeli waliamriwa. Na tayari tumechukua hiyo, ya kuchinja mwana-kondoo.

44 Mungu alikuwa akilileta kanisa Lake katika kutoka, kulitoa kutoka Misri, kuingia katika nchi ya ahadi. Naipenda hiyo. Walikuwa wakivuka, kuimiliki nchi. Mungu aliwapa hiyo nchi, na hata hivyo ilikuwa imezingirwa na majengo marefu makubwa na nyua. Na kuta kuzunguka Yeriko, magari ya farasi yangeweza kufanya mashindano ya mbio kuuzunguka. Na hebu wazia tu hilo, hata hivyo, Mungu alisema, "Nimekupa wewe. Ni yako." Lakini walilazimika kusafisha, kuusafisha.

45 Na hivyo ndivyo Mungu amefanya leo. Amempa kila mmoja wenu, anayetaka jambo Hilo, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Lakini huna budi kuingia, kumiliki, hivyo tu; pambana na tofauti, na kubomoa kuta, na uanze mle ndani na kulipata.

46 Unasema, "Mchungaji alisema, 'Si kwa ajili yetu leo.'" Tembea tu moja kwa moja kupita hiyo. "Mama alisema, 'Nitakufukuza kutoka nyumbani.'" Nenda moja kwa moja upite hiyo. "Mume alisema, 'Nitakuacha.'" Nenda moja kwa moja upite hiyo. Ni hayo tu. Huna budi kwenda na kuimiliki! Ni hayo tu.

47 Uponyaji wa Kiungu ni kwa ajili ya kila mmoja wenu. Kila mmoja wenu anayeketi hapa usiku wa leo, akiwa na kansa, shida ya moyo, chochote kile, Mungu ametoa ahadi. Na ni yako, lakini huna budi kwenda na kuimiliki.

48 Sasa unasema, "Vema, sijisikii vizuri tu." Hiyo haina uhusiano wowote nayo. Ahadi ni yako. Mungu alikupa. Ingia tu moja kwa moja na uwaue Wafilisti, kutoka upande mmoja hadi mwingine. Na kuwatoa Wahivi wote na—na Waamori, waue tu. Ingia moja kwa moja ndani, ichukue. Mungu alisema, "Ni yako. Nenda kaichukue."

49 Lakini hakusema, "Sasa, nitaingia, nifagilie yote, na kuwajengea miji mizuri, na kuwaweka kwenye barabara rahisi." Hafanyi hivyo.

50 Anakupa, nawe una jambo la kufanya. Ni mzuri wa kutosha kukupa nchi, alisema atakusaidia na kuwa nawe. Nenda, ichukue!

51 Na kama wewe ni mgonjwa, usiku wa leo, kilema, kipofu, kiziwi, bubu, chochote ulicho; nenda, ichukue. Mungu alisema ni yako. Ni milki yako. Mungu alikupa.

52 Aliwaambia kwamba angewapa nchi hiyo. Akamtuma Malaika mbele yao, kuisimamia njia, na kuwaleta mahali pale.

53 Waangalie hao wapelelezi walipokwenda kule. Hawa hapa kumi wao wakirudi, wakasema, “Loo, hatuwezi kufanya hivyo. Haiwezekani. Mbona, sisi ni wanasayansi, na tumeangalia jambo hilo kabisa. Haiwezekani kisayansi. Hatuwezi kuifanya.”

54 Lakini kulikuwa na jamaa wawili, mmoja wao aliyeitwa Yoshua, na mmoja aliyeitwa Kalebu. Hawakuwa wakiangalia upande wa kisayansi ulikuwaje. Walikuwa wakiangalia kile ambacho Mungu alisema. Kasema, “Tunaweza.” Na hiyo ni kweli. Na wakarudisha ushahidi fulani kwamba ilikuwa nchi nzuri.

55 Nimefurahia sana ushahidi huo, (nanyi je?) kwamba kuna Nchi nzuri juu yetu! Na tuko njiani, usiku wa leo. Haleluya! Sawa.

56 Hawa hapa, sasa, kabla tu ya ukombozi. Mungu alihitaji wana wa Israeli, kwamba wangelindwa kwa hakika, ili wamchinje mwana-kondoo huyu. Na kuweka damu kwenye kizingiti cha juu, juu ya mlango, namna *hii*, na kila mwimo.

57 Nao walipaswa kuingia na kumla mwana-kondoo huyu, kila sehemu yake; angalia, mwana-kondoo wote, si sehemu yake tu. Kila sehemu yake ilikuwa iliwe.

58 Baadhi ya watu wanasema, “Nitachukua tu sehemu *hii*, na nita—nitaamini sehemu *hii*.” Bali huna budi kuyachukua yote, kila sehemu Yake. Sema, “Loo, ninaamini alijeruhiwa kwa makosa yetu, lakini, ‘kwa kupigwa Kwake,’ sijui juu Yake.” Tunataka Yote. Kila sehemu Yake italiwa; Yote. Baadhi Yake inakuwa ngumu, lakini inatubidi kuila, hata hivyo. Mungu alisema hivyo.

59 Angalia kifungu cha 10 sasa.

> *Wala msi—msisaze kitu chake chochote hata*... *asubuhi; bali kile* kitakachosalia...*hata asubuhi*... *mtakichoma kwa moto*.

60 Na, sasa, haitasalia chochote; kila kitu. Sasa, alisema, “Mnapoila, msiile mbichi, wala ya kutokoswa majini, lakini lazima muile ikiwa imeiva vizuri.” Na mimi napenda hiyo.

61 Watu wakijaribu kula Neno la Mungu, nao wanalichukulia kana kwamba ni bichi; wanalitafuna, na kulitemea mate, na kila kitu kingine. Wanasema, “Loo, siwezi kabisa kulichukua. Siwezi kustahimili Hilo.” Halijapikwa vya kutosha. Ni hayo tu.

62 Alisema, “Iokeni kwa moto.” Moto unawakilisha Roho Mtakatifu. Umweke Mungu moyoni mwako, kwanza, naye atakupikia. Hiyo ni kweli. Imepikwa, imekamilika, imekolezwa, basi ina ladha nzuri.

63 Sasa, huwezi kusimama *hivi*, nje, useme, “Loo, mimi, sijui kama ni kwa ajili yangu, ama sivyo. Hiyo inaweza kuwa kwa ajili ya siku zilizopita.” Mpate tu Roho Mtakatifu, kwanza, na uone kile uponyaji wa Kiungu unachomaanisha kwako basi.

64 Uone kile dini ya moyoni inachomaanisha kwako basi, unapokuwa na Roho Mtakatifu hapa wa kumpika Mwana-Kondoo anapokuja. Amina. Hiyo ni kweli. Mpike Mwana-kondoo, kwanza. Na inabidi uwe na Moto ili kuipika nao. Inapaswa kuokwa. Loo, jamani, hapo ndipo inapokuwa nzuri. Ioke, inachoma tu na kuondoa ninii yote . . .

65 Nilikuwa nimesimama hapa, si muda mrefu uliopita, karibu na mtambo mkubwa wa kuyeyusha, na nikaona jinsi moto ule ulivyokuwa mkali, na ilipikwa tu na kupikwa na kupikwa. Na kadiri ilivyozidi kuwa moto, ndivyo ta—takataka kwenye chuma, katika dhahabu, zote zilikuja juu, nao wakaziondoa. Na wangeongeza ukali wa moto zaidi kidogo kwenye kiyeyushi. Na basi wakati hili lingechemka zaidi, wangepata vitu vingine tofauti zaidi, kimbwi na kadhalika, kutoka kwayo.

66 Ya kwanza kuja juu ilikuwa uchafu, kama uchafu na matope. Kilichofuata kilikuwa madini kama, loo, kitu kisichokuwa kizuri; baadhi ya fedha za haraka, na mambo haya yote, wanakuja, na kuyaondoa hayo. Wakashuka, moja kwa moja, na kitu cha mwisho walichotoa humo kilikuwa ni kimbwi. Hiyo ni dhahabu ya mpumbavu.

67 Unajua kuna mambo mengi ndani ya watu ambayo hujaribu kudanganyana wakati wewe ni Mkristo, ama kuiga, hata hivyo. Unaona? Bali mwache tu Roho Mtakatifu achemshe na kuondoa kila kitu, toa—inaondoa dhahabu yote ya mpumbavu kutoka kwako, pia.

68 Dhahabu ya mpumbavu, watu wengi wanaenda Magharibi na wanapata baadhi yake, nao wanafikiri, loo, walipata mgodi wa dhahabu. Inang'ara vizuri kuliko dhahabu. Lakini ni dhahabu ya mpumbavu, haina thamani yoyote kwake.

69 Na sasa wanaipika hiyo, na wanaifuta yote, na kuendelea tu kuipika na kuipika, mpaka iwe dhahabu safi, iliyochemshwa hadi si kitu ila dhahabu tupu.

70 Na hivyo ndivyo Mungu afanyavyo katika Kanisa Lake, humimina Roho Mtakatifu juu Yake, na anapika humo ndani mpaka anatupilia mbali ulimwengu wote, na tofauti, na ubinafsi, na haya yote, mpaka aichemshe tu kutoka kwa kila mtu atakayekuja Kwake. Amina.

71 Sasa, basi, unaweza kula. Hapa kuna wazo lingine zuri hapa, kwenye—kwenye aya ya 11.

> *Tena mtamla hivi; mtakuwa* . . . (sikiliza hili) . . . *mmefungwa viuno vyenu,* . . . (Naipenda hiyo) . . . *mmevaa viatu vyenu miguuni,* . . . *fimbo zenu mikononi mwenu; nanyi mtamla kwa haraka;* ni *pasaka ya* BWANA.

72 Naipenda hiyo. Wakati unapokula, uwe tayari kwenda. Hilo ndilo suala.

73 Hebu tugeukie Waefeso, yapata mlango wa 6 wa Waefeso, na tuangalie humu ndani kile ambacho Paulo alisema kuhusu kuliweka Kanisa tayari; mlango wa 6 wa Waefeso, kuanzia kifungu cha 14 cha mlango wa 6.

> *Basi simameni, hali* mmejifunga *kweli viunoni,* . . . *mmevaa dirii ya haki kifuani;*
>
> . . .*mmefungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani;*
>
> Na *zaidi ya yote* mkiitwaa *ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima*. . .*mishale yenye moto ya waovu.*
>
> *Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu:*

74 Ona Paulo akimvisha mtu kwa ajili ya uwanja wa vita, kwa ajili ya safari.

75 Mungu, hapo mwanzo, katika kuwakomboa Israeli, alisema, "Sasa mnapaswa kujiandaa kwa safari. Mnapokuja chini ya damu, vaeni viatu vyenu. Jifungeni viuno. Shikeni fimbo zenu mkononi na mwe tayari kwa wito." Naipenda hiyo.

76 Mtu sasa, anapoingia ndani ya Kristo, huvaa viatu vyake vya Injili, kuhubiri Injili; amevaa kofia ya wokovu; dirii ya haki kifuani; hujifunga kiunoni. Kuna . . .

77 Kawaida, katika askari wa zamani, walipovaa mapambo hayo ya vita, walikuwa na ukanda mkubwa. Walikuwa wameifunga pamoja, wakiwa wameshikilia juu ya viuno vyao, ngao hizi, kuzuia mikuki ya adui. Ni somo la kweli jinsi gani hilo lililo kwetu. Na wakati ki—kiuno kinaanza kuwa dhaifu, kinaning'inia chini, ngao, wangeweza kukaza juu ya mkanda wao, kuikaza tena.

78 Ni picha nzuri jinsi gani, leo, unapoanza kujisikia kama unalegea, au ibilisi anasema, "Haina maana." Nyosha mkono na ukaze ukanda kidogo; vuta upanga kwa nguvu kidogo mkononi, na usonge mbele. Naipenda hiyo, uwe tayari kwa safari.

79 Kila mtu akitembea chini ya damu hiyo, usiku huo, aliamriwa kukaa pale, asitoke nje mpaka amri zije, kuondoka.

80 Na kila mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, anaingia ndani ya Kristo, ana Uzima wa milele; huvaa ngao yake, dirii yake, akisimama tayari, na amekatazwa kuondoka mpaka iamrishwe kuondoka.

81 Loo, si ni ajabu? Hivi hamna furaha kwamba mmezifunga zote, usiku wa leo, ninyi askari?

82 Tulikuwa na kiongozi wa nyimbo kwenye maskani, wimbo wetu wa mada ulikuwa:

Vita vimepamba moto, Enyi askari Wakristo,
Uso kwa uso katika safu kali,
Na silaha zinazong'ara, rangi zinatiririka,
Haki na batili zinakabiliana leo;
Vita vimepamba moto, ila msichoke,
Iweni na nguvu na katika nguvu Zake shikilieni kwa uthabiti;
Mungu akiwa upande wetu, bendera Yake juu yetu,
Hatimaye tutaimba wimbo wa mshindi.

83 Wengi wao watakatifu wa zamani wamekwenda kaburini. Lakini moja ya siku hizi, kule katika ulimwengu mpya, watakapokuja kwenye Nchi ya ahadi, bendera ya msalaba itakuwa juu yetu, na tutaimba wimbo wa mshindi. Tunapoketi kwenye Karamu ya Arusi usiku huo, kuzunguka meza, ile meza kuu, labda urefu wa maili laki moja, huku watakatifu waliooshwa kwa Damu wameketi kuzunguka pale. Ninataka kushuka kwenye meza na kusalimiana kwa mikono na kila mmoja wao, amina, nikipaza sauti tu. Unataka kunisikia nikipiga kelele? Ngoja mpaka nifike huko; niangalie. Mimi si mkubwa vya kutosha, bado, kwa hili.

Lakini, angalia, kwenye safari sasa. Jitayarishe. Tunaenda.

84 Hapa kuna picha ya kusikitisha, kabla hatujafika kwenye somo letu la kawaida, inapatikana katika mstari wa 38 hapo. Sikiliza.

> *Na kundi la watu waliochangamana wakakwea* pamoja na kundi lao . . .

85 Hapo ndipo Israeli walifanya kosa. Miujiza ilikuwa imefanywa. Watu ambao hawajaongoka walifuata kwa sababu ya nguvu za kimbinguni, hatimaye waliwaingiza kwenye matatizo. Na kuendelea chini, tutaona hapa, katika yapata aya ya 42 na aya ya 43. Bwana akinena na Musa, akasema, ya kwamba, "Hakuna ila wale waliotolewa kafara . . . wangeweza kula sadaka," hasa, "bali wale waliotahiriwa. Hakuna wageni, hakuna wa nje, hakuna mtu anayepaswa kuipokea isipokuwa wale waliotahiriwa."

86 Na ni fedheha jinsi gani tuliyo nayo leo, katika siku hii, marafiki wapendwa; kwamba wakati, katika kanisa, kila mtu ambaye ni mfuasi wa kanisa anakula ushirika. Na hilo ni kosa. Ni wale tu waliokombolewa, hao tu ndio wanaostahili.

87 Isaya alinena na kusema, "Meza za Bwana zitajaa matapishi." Kasema, "Nitamfundisha nani Mafundisho? Wale walioachishwa kunyonya matiti." Kasema, "Amri lazima iwe juu ya amri; mstari juu ya mstari; huku kidogo, na kule kidogo." "Na ushikilie sana lililo jema." Mungu akinena, akijua ya kwamba siku tunayoishi, ya kwamba kanisa lingekuwa la kisiasa sana, mpaka wangeruhusu kila kitu, watu, kuingia; mradi tu walikuwa

na jina lao kwenye kitabu cha kanisa, walikuwa washiriki, walikula ushirika.

88 Na Biblia ilisema, "Alaye na kuinywa, isivyostahili, ana hatia ya mwili na Damu ya Bwana."

Yohana Mtakatifu, mlango wa 13, Yesu akizungumza.

89 Wakorintho wa Pili mlango wa 11, Paulo alisema, miaka mingi baadaye, ya kwamba, "Anayekula na kunywa hii, isivyostahili, atakuwa na hatia ya mwili na Damu ya Bwana. Mtu na ajichunguze mwenyewe," anasema, "kabla hajala." Ninanukuu Maandiko. Hiyo ni kweli. "Alaye na kunywa, isivyostahili, anakula na kunywa hukumu kwa nafsi yake mwenyewe, kwa kutokuupambanua mwili wa Bwana. Na kwa sababu hii wengi wa kwenu ni wagonjwa na dhaifu, na wengi wamelala." Hakikisha unasimama sawa na Mungu.

90 Hii hapa katika kivuli, kwamba, hakuna mtu ila wale waliotahiriwa! Haidhuru alikuwa mwaminifu jinsi gani, jinsi alivyolisaidia kanisa la Kiyahudi; ilibidi awe mwongofu, ilibidi awe mwaminio halisi aliyetahiriwa, kabla hajaweza kula ushirika, ama kula pasaka. Loo, jinsi tulivyotoka kwenye mstari leo!

91 Sasa twende haraka, basi. Na Mungu akawatoa usiku wa leo. Tunafungua sasa kifungu cha 13 cha mlango wa 14.

92 Mungu aliwapa Nguzo ya Moto kuwatangulia. Nafikiri walikuwa na picha hapa, usiku wa leo. Nami nasema kwa heshima. Kwa maoni yangu ya uaminifu, tukiwa hapa katika kundi hili usiku wa leo, ninaamini Hilo li pamoja nasi usiku wa leo. Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli, inatangulia mbele yetu, ikifanya ishara zile zile na maajabu. Na mwalimu yeyote hapa, ama msomi wa Biblia, anajua ya kwamba Malaika aliyewafuata Israeli na kuwaongoza hadi nchi ya ahadi, alikuwa ni Malaika wa Agano, ambaye alikuwa ni Yesu Kristo.

93 Na, leo, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele" anafuata mbele ya kundi hili mnalotaka kuwaita watakatifu wanaojibingirisha, kama mnataka kufanya hivyo. Sawa. Inaendelea, ikiongoza kutoka ushindi hadi ushindi! Mungu asifiwe!

94 Katika mataifa hayo, katika siku hizo, walidharauliwa na kuchukiwa na kukataliwa, na kukataliwa na mataifa, na kuitwa kila kitu.

95 Ndivyo ilivyo leo, kwa mwaminio wa kweli. Ninyi, katika makanisa yenu, mnajua, unapochukua msimamo kwa ajili ya Kristo na kuitetea Kweli, kanisa zima linasema, "Mwangalie! Amerukwa na akili. Amekuwa wazimu." Unaona?

96 Usizingatie hilo. Endelea kufuata. Umejihami kabisa sasa. Nayo Damu inakutangulia; Roho Mtakatifu akikuongoza. Endelea tu kusonga mbele. Usizingatie kile ambacho mtu yeyote

anakuambia. Tazama moja kwa moja kuelekea Kalvari, na uendelee mbele. Mfano mzuri!

97 Sasa, walikuwa wametoka, wakamaliza, na kupata . . . Na sasa angalia, ukombozi wa damu uliwatoa Misri, sasa ilibidi wawe na kitu kingine sasa cha kuwapeleka hadi nchini. Sasa ndio wanaanza kuanza. Walikuwa wametoka, wametahiriwa, wakaja chini ya damu, na wako safarini. Sasa walikuwa wamefikia kitu fulani. Walikuwa wakienda huko, wakijua ya kuwa walikuwa wamepita kutoka mautini kuingia uzimani; walijua walikuwa na Uzima wa Milele.

98 Lakini hawa hapa, wanakuja sasa, na shida inaanza kuinuka. Hili hapa jeshi la Farao linakuja, likiwafuata, kuwakamata. Shida ikaingia.

99 Sikiliza! "Mungu ni kimbilio letu na nguvu zetu, msaada ulio karibu sana wakati wa shida." Loo, natumaini unaona hili. Unaona? Hii hapa. Jua . . . Lakini, nikisikiliza, kifungu cha 13 sasa.

*Musa akawaambia watu, Msiogope, . . .*

100 Napenda hiyo. Baada ya Yesu kufufuka kutoka kwa wafu, Maneno yake yalikuwa daima, "Msiogope."

101 Hiyo ndiyo shida ya Kanisa leo, linahofia sana kwamba utashindwa. Unawezaje kushindwa ukiwa ndani ya Kristo? Huwezi kushindwa. Una Uzima wa milele. Mashetani wote katika kuzimu hawawezi kukutetemesha. Una Uzima wa milele. Yesu alisema hivyo. Kwa hivyo usiogope kushindwa.

102 Unasema, "Kweli, ninahofia nitaingia ushupavu." Ni afadhali niwe na ushupavu kidogo kuliko kutulia bila kufanya lolote. Hakika ningefanya hivyo. Mtu atakayefanya jambo . . .

103 Inasimuliwa kuhusu Ballard hapa juu, jamaa alikuja kutafuta kazi kutoka kwake, naye akasema, "Saini jina lako hapa." Akachukua penseli yake, kutia sahihi. Akasema, "Wapi kifutio chako?"

Kasema, "Mimi sininii . . . sifanyi makosa."

Akasema, "Siwezi kukutumia; hutafanya lolote."

104 Hiyo ni kweli. Hufanyi makosa, hufanyi—hufanyi chochote. Twende, ndugu. Amka na kwenda. Nampenda Longfellow hapo:

Usiniambie, kwa nyimbo za maombolezo,
Maisha ni ndoto tupu!
Na nafsi inayolala imekufa,
Wala mambo hayako yanavyoonekana.

Alisema:

Naam, maisha ni halisi! Na maisha ni amana!
Wala kaburi siyo kikomo chake;
Wewe ni mavumbi, unarudi mavumbini,
Haikunenwa juu ya nafsi.

Na tuamke tukatende kazi,
Kwa moyo kwa ugomvi wowote;
Usiwe kama ng'ombe bubu, wanosukumwa!
Kuwa shujaa!

105 Usisubiri watu wakushawishi kwa Kristo. Simama kama mwanamume ama mwanamke, mkubali Yeye, na uende mbele katika ushindi. Amina. Hivyo ndivyo Mungu anataka, askari wakali, walio tayari. Huenda usiwe, una uzito wa pauni mia moja na tano, lakini bado unaweza kuwa mwekundu, ndugu, na umejaa nguvu, ikiwa tu utamwacha Mungu apate njia Yake. Nimewaona watu wenye uzito wa pauni mia mbili, hawakuwa na hata wakia wa mtu ndani yao. Hiyo ni kweli. Vema. Angalia.

> . . .*Musa akawaambia watu, Msiogope*. . .*simameni imara, mkauone wokovu wa* B*WANA*, . . .

106 Hilo ni jema. Endelea tu. Usiogope kuhusu chochote. Ikiwa umemkubali Kristo kama Mwokozi wako, endelea.

107 "Ndugu Branham, ninataka ubatizo wa Roho Mtakatifu." Endelea tu kusonga mbele. Usiogope.

108 Unasema, "Mimi ni mgonjwa sasa, Ndugu Branham. Siwezi kwenda mbali zaidi." Usichoke. Endelea tu kusonga mbele; uone wokovu wa Bwana wetu! Kubali. Endelea tu.

109 "Je, itakuwaje? Daktari alinikataa." Sasa, jamaa huyo amefanya vizuri sana alivyoweza, lakini Mungu hajafanya vizuri sana awezavyo bado. Hiyo ni kweli.

110 Hebu kidogo tu, msikilizeni sasa. Vema.

> . . .B*WANA*, atakayowaonyesha *leo: kwa ajili ya Wamisri* (washambulizi, kweli-. . .mleta shida) . . .

111 Unasema, "Ndugu Branham, laiti ningeweza tu kuacha kuvuta sigara! Laiti ningeweza tu kuachana na unywaji pombe! Laiti ningeweza tu kuacha wizi wangu! Kama ningeweza tu kuacha kufanya *hivi, vile,* na *vingine*." Usichoke. Endelea tu. Mungu atashughulikia hayo mengine.

112 "Kama ningalijua ningeweza kufanya jambo hilo, Ndugu Branham, ningemkubali Kristo sasa hivi." Usiwe na wasiwasi. Endelea. Endelea tu. Utauona wokovu wa Bwana!

> . . .*kwa maana hao Wamisri mliowaona leo hamtawaona tena milele*. (Amina. Itasuluhishwa, baada ya kitambo kidogo.)

> B*WANA atakupigania, na* wewe utakuwa ninii . . .*kaeni kimya*.

> B*WANA akamwambia Musa, Mbona unanililia mimi? sema na wana wa Israeli, kwamba wasonge mbele:* (Napenda hilo.)

113 Usijaribu kusema, useme, "Vema, nilijiunga na kanisa, miaka kumi iliyopita, Ndugu Branham. Nimekuwa mshiriki

mzuri mwaminifu." Hilo ni sawa; nashukuru kwa hilo. Lakini hebu tusonge mbele, usiku wa leo. Mungu anaendelea. Watu leo hii, hapa, wanarudi nyuma, wanasema, "Vema, sasa . . ."

114 Sayansi, miaka mia moja na hamsini iliyopita; kulikuwa na sayansi huko Ufaransa, ambayo ilisema, "Ikiwa mtu aliwahi kwenda mwendo wa kutisha wa maili thelathini kwa saa, nguvu za uvutano zingemwondoa duniani, na angekuwa ameenda." Huh! Maili thelathini kwa saa? Anaenda kama maili elfu moja na mia sita kwa saa sasa. Kamwe husikii sayansi ikirejelea jamaa huyo. Alikuwa sawa katika siku yake, lakini wanaishi katika siku nyingine. Hiyo ni kweli.

115 Lakini, sisi wahubiri, loo, la. "Uponyaji wa Kiungu? Sasa ngoja nione kile—kile Mtakatifu Moody, Finney, Knox, Calvin, baadhi yao walichosema juu Yake." Walikuwa sawa katika siku zao. Lakini tunaendelea, tunasonga mbele. Tuna kitu kingine.

116 Yesu alisema, katika mfano pale, wa mpanzi, wakati mpanzi alipotoka na kupanda mbegu. Na baadhi . . . Adui akaja na kupanda magugu kwenye ngano. Alisema, "Ziacheni zikue pamoja."

117 Siku zote unaonyesha jinsi ulimwengu unavyozidi kuwa mbaya, lakini unashindwa kuona jinsi Kanisa linavyokuwa na nguvu, wakati huo huo. Anainuka, akisimama uwanjani. Loo, Yeye ni kundi dogo, lakini, ndugu, Mungu yu pamoja Naye. Naye atashinda kwa hakika kama vile Kristo alivyofufuka kutoka kwa wafu. Amina. Kanisa la Mungu halitashindwa kamwe. "Malango ya kuzimu hayatalishinda." Ilionyesha yangekuwa dhidi Yake, lakini hayawezi kushinda. Kanisa litashinda, kwa Damu ya Yesu Kristo, kwa gwaride la ushindi. Nina hakika na jambo hili moja, ya kwamba Mungu atakuwa na Kanisa lisilo na doa, kunyanzi, ama waa. Amina. Nina furaha sana kuhusu hilo.

118 Sasa, "Ikiwa niko katika Kanisa hilo." Amina. "Ndugu Branham, unaingiaje ndani Yake, kwa barua?" Hapana. "Je, unaingiaje ndani Yake?" Kwa Kuzaliwa; kuzaliwa ndani Yake!

119 Nimekuwa katika familia ya Branham, itakuwa miaka arobaini na mitano, siku ya sita ya Aprili hii ijayo, na hawakuwahi kuniomba nijiunge na familia yao. Nilizaliwa Branham. Daima nitakuwa Branham.

120 Nilizaliwa Mkristo, katika Yesu Kristo. Nitakuwa Mkristo, maana Mungu ameliweka hivyo, kwa uteuzi. Alituita, kwa neema ya Mwanawe Mwenyewe mpendwa. Tulimkubali na tukapata Uzima wa Milele. "Kwa kupeana mkono kumoja"? "Kwa uanachama mmoja"? "Kwa barua moja"? "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, Yesu Kristo," na hapo tukawa raia wenzi wa Ufalme.

121 Nilikuwa nawaza leo, nilipokuwa mbali nikiomba, kwamba jinsi ambavyo hii ndiyo siku ambayo tutalazimika kuwajibikia. Sitalazimika kuwajibikia kizazi kilichokuwa kabla yangu, au

kizazi kitakachokuwa baada yangu. Lakini, katika Hukumu, nitasimama pamoja na kizazi hiki. Nami nikasema, “Angalia pale, picha ya mwanamke kwenye bango, akinywa bia, kitu fulani, alisema alikuwa ‘bila pumzi,’ au kitu fulani.” Nikasema, “Ndiyo, na bila Uzima, pia.” Vema. Haya basi. Nikasema, “Ni fedheha iliyoje!”

122 “Pamoja na mahubiri yote,” nilisema, “wakati mwingine inaonekana,” nilimwambia mke wangu, nikasema, “wakati mwingine inaonekana hayana mafanikio yoyote. Lakini sina budi kuwa ndiye sauti ya onyo, kwa vyovyote vile, haidhuru watu wanafanya nini juu yake. Sina budi kuhubiri Injili, kwa vyovyote vile, na kutoa ushuhuda wa ufufuo na Nguvu za Yesu Kristo.” Na waliache, na wageuze migongo yao; Mungu atawahukumu kwenye Hukumu kwa ajili yake. Ninawajibika tu kwa kuhubiri, na wahudumu wengine pia, wanaohubiri Injili.

123 Sasa, ninaipenda tu. Angalia, “Endeleeni mbele sasa,” nanyi mtauona utukufu wa Mungu. Lakini, sikilizeni, kifungu cha 16 sasa. Tunasoma hili.

*Nawe inua . . .juu fimbo, . . .*

124 “Fimbo,” hiyo ilikuwa fimbo ya hukumu. Sasa, haikuwa fimbo ya Musa. Hiyo ilikuwa fimbo ya Mungu. Kama utaangalia, Musa, alichukua hiyo fimbo, akaiinua *hivi,* viroboto wakaja. Aliishikilia juu ya maji, ikageuka kuwa damu. Ilikuwa ni fimbo ya hukumu ya Mungu. Na fimbo iyo hiyo . . .Ipate! Fimbo iyo hiyo ndiyo aliyoipiga nayo mwamba; ukaja ufa katika ubavu wa mwamba, maji yakatoka katika mwamba huo.

125 Sasa, mwamba huo ulikuwa ni Kristo, na ilikuwa ni hukumu ya Mungu. “Siku utakapokula, siku hiyo utakufa.” Alimpiga Kristo pale Kalvari, na kulipa kifo hicho kichungu, na maumivu. Hakuna mtu, ambaye angeweza kamwe kueleza ilivyokuwa, au kamwe hatawahi. Hapo Mungu akaweka hukumu yote ya Kiungu juu Yake, na kumpiga ubavuni, wakati kutoka ubavuni Mwake yalitoka maji na Damu na Roho, kwa ajili ya ukombozi wetu.

126 Jinsi watu wanavyochora picha Yake, wakati mwingine, akiwa amejifunika kanzu, ama kitu fulani, msalabani. Hivyo sivyo. Walimtupia Mtu huyo, kila kitu kichafu na kiovu walichoweza; lakini ilimbidi awe. Huyo hapo, aliye mkuu na mwaminifu zaidi kuliko ulimwengu wote, aliyepata kuwako au atakayekuwako. Na kisha kuanikwa, uchi, msalabani; amejeruhiwa, akapigwa, anatokwa damu; mate ya dhihaka yakining’inia usoni Mwake; taji ya miiba ya dhihaka juu ya kichwa Chake. Lakini hapo ndipo Yeye alishinda mauti, kuzimu, dhambi, ugonjwa, na kaburi, na kulipa gharama kwa ajili yetu sote.

127 Inasemwa mara nyingi, wakati mwingine, “Hapo ndipo alipotolea uchungu wa mauti.” Hapo ndipo Paulo alisema, “Ewe mauti, u wapi uchungu wako?”

128 Nimeambiwa ya kwamba wadudu wengi, nyuki na kadhalika, wana mwiba, na ni sumu, wakiwa nao. Lakini wakati mmoja wanapouma, wanapoteza mwiba wao.

129 Mauti ilikuwa na mwiba ndani yake, wakati mmoja; lakini Kristo, pale Kalvari, aliutoa mwiba kutoka katika mauti. Haleluya! Loo, ninapowazia jambo hilo! Hapo ndipo alipotoa mwiba kutoka katika mauti, kwa ajili yangu na wewe, uchungu wote wa mauti.

130 Paulo alisema, walipokuwa wakienda kumkata kichwa, katika gereza la Kirumi, alisema, “Kifo, u wapi uchungu wako?” Ilielekeza nyuma Kalvari, na hapo ndipo mwiba ulipotolewa kwenye mauti. “Kaburi, u wapi ushindi wako?” Akasema, “Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.” Amina. Vema.

> *. . .fimbo* (hukumu), *na inyooshe. . .*kufunika *ba—bahari, na kuigawanya: nao wana wa Israeli* watapita *kati ya bahari katika nchi kavu.*
>
> *Nami, tazama, nitafanya* moyo *wa Wamisri kuwa mgumu, nao watawafuata: nami nitajipatia utukufu kwa Farao, na kwa jeshi lake lote,* na *kwa magari, na kwa wapanda farasi.*
>
> *Na Wamisri watajua ya kuwa mimi ndimi Bwana,* nami *nimejipatia utukufu kwa Farao,* na *kwa magari yake, na wapanda farasi wake.*
>
> *Kisha malaika wa Mungu, . . .*

131 Sikiliza! Kaza kamba sasa. “Naye Malaika wa Mungu, aliyetangulia mbele ya jeshi la Israeli,” Bado yuko hapa.

> *. . .malaika wa Mungu, aliyetangulia mbele ya jeshi la Israeli, akaondoka,* akarudi *nyuma yao; na ile nguzo ya wingu ikaondoka hapo mbele ya nyuso zao, ikasimama nyuma yao;* (ama, alipanda kutoka *hapa*, na kusimama *hapa* nyuma; mpatanishi katika wakati wa taabu.)

132 Wakati shida inapoanza kukukabili, magonjwa kila upande, shida, Malaika wa Mungu anakuja, anatokea katikati yako na magonjwa, na kusimama hapo njiani, huku akikusahi kuchukua Neno la Mungu.

133 Mungu alikuwa amewapa Israeli ahadi, ya kwamba wangeingia katika nchi. Kulikuwa na milioni moja, labda, ya watu, wakija, kuwafuata na kuwaangusha chini, na kuwakatakata, kama kundi la wanyama. Lakini Malaika wa Bwana, aliyekuwa pale kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi, akainuka kutoka kambini akaenda na kusimama kati yao na hatari.

134 Haleluya! Bado anafanya hivyo. Atafanya njia. Loo, ninampenda tu kwa sababu hiyo, sivyo? Atafanya njia kwa kila mgonjwa anayeketi hapa sasa hivi. Amekwisha tengeneza njia, na amesimama kati yenu na shida.

135 Nami najua yuko hapa sasa hivi. Unaweza kuniita mshupavu ukitaka; Siwajibiki kwa yale unayosema. Lakini ninawajibika kwa yale ninayosema, mbele za Mungu. Lakini Yeye Yule aliyewaongoza wana wa Israeli, kama nimelihukumu vyema, juu ya Nuru hiyo mnayoiona usiku wa leo, au mliyoona kwenye hiyo picha. Nadhani wameziweka nje usiku wa leo. Malaika yuyo huyo wa Mungu yuko ndani ya jengo hili sasa hivi, kufanya vile hasa Yesu alivyofanya katika siku hiyo. Yuko hapa kuthibitisha. Yale tu aliyofanya wakati huo, Yeye yuko sasa, na atakuwa vivyo hivyo daima. Malaika wa Mungu, akipanda kusimama kati yetu na ugonjwa, kusimama kati yetu na mauti.

136 Si ajabu Daudi alisema, "Naam, nijapotembea kati ya mabonde ya uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya: kwa maana Wewe u pamoja nami." Hakika.

137 Akasimama pale, Malaika wa Mungu akatangulia mbele ya kambi ya Israeli, akaondoka, akaenda na kusimama kati yao na adui.

138 Naye Malaika wa Mungu amesimama, usiku wa leo, kati ya kila mtu binafsi hapa na adui. Ninajua ninachozungumzia. Ninajua, nikiwa nimesimama hapa jukwaani sasa, mbele ya kundi hili dogo la watu usiku wa leo, ninajua ya kwamba Mungu amejishusha, akishuka kutoka Utukufuni, na kusimama katika jengo hili sasa. Iwapo utathubutu tu kuhamia Neno la Mungu, uone kama hatasogea mbele yako. Tazama.

139 Ikaja kati ya kambi na Wamisri. Anakuja kati yako na ugonjwa wako. Yeye anasimama kati yenu na dhambi zenu, sasa hivi. Kwa nini? Tuko katika kutoka kwa Kanisa. Misri daima iliitwa ulimwengu, na wakati Israeli ilipotoka . . . Kumbukeni, walikuwa washiriki wa kanisa kule chini. Lakini baada ya ile damu na upatanisho kufanywa, wakawa watahiriwa wa Mungu.

140 Na tohara, leo, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. "Wote," alisema Stefano, "ninyi nyote msiotahiriwa mioyoni na masikioni, kwa nini kila mara mnampinga Roho Mtakatifu? Kama baba zenu walivyofanya, nanyi pia." Roho Mtakatifu akitahiriwa moyoni, akikatilia mbali mambo ya ulimwengu. Ilikuwa ni kanisa la mtindo wa kale la utakatifu liliishi hivyo, lilitenda kama hilo, liliishi kama hilo. Lakini, leo, ni kama tu kwingineko ulimwenguni. Ni aibu. Tumelegeza kamba.

141 Maskini Ndugu Spurgeon alizoea kusema, mhubiri mzee wa Methodisti rafiki yangu, alikuwa akiimba wimbo:

Tulilegeza kamba, tulilegeza kamba,
Tulipatana na dhambi.
Tulilegeza kamba, kondoo wakatoka nje,
Mbuzi waliingiaje?

142 Kwa sababu umelegeza kamba! Ndivyo ilivyo. Umeshusha kiwango cha maisha ya Kikristo, kwa sababu seminari ziliangua wahubiri wachache na kuwatuma ili wapatane na Kweli. Lakini Roho Mtakatifu daima amekuwa pale kuhukumu dhambi, na usiku wa leo amesimama kati ya mwaminio na mambo ya ulimwengu. Amina.

> *Ikafika kati ya kambi* na *Wamisri na jeshi la Israeli; nalo lilikuwa wingu* la *giza kwao, lakini liliwaangazia hawa usiku; hivi kwamba mmoja hakumkaribia mwingine usiku kucha.*

143 Angalia, kitu kile kile kilichopewa kundi *hili* la waaminio, Nuru, ilikuwa ikiwapofusha.

144 Vema, vaeni jaketi zenu za kuzuia mshtuko. Hii hapa inakuja. Tazama, kila mtu anayeikataa Nuru anakuwa kipofu na anatembea gizani kwa sababu hukubali Nuru. Amina. Mungu hutuma wahudumu wanaohubiri Injili. Yeye hutuma ishara na maajabu miongoni mwa wanadamu, ili kuithibitisha kuwa ni Kweli; na watu wanaikataa, hakuna lililosalia ila giza kwako. Tembea katika Nuru wakati Nuru ikiangaza, ndugu yangu. Pokea Nuru. Kristo ndiye Nuru. Amekuja kukuletea Nuru. Lakini wale walioikataa Nuru walipokea giza. Na kila mwanamume na mwanamke, usiku wa leo, anayeikataa Nuru, anatembea gizani, bila kujua anakoelekea. Anayumbayumba akiwa mzuri sana, anayependwa na watu, lakini sijui anasimamaje katika Uwepo wa Mungu.

145 Iangalie! Ni jambo la ajabu jinsi gani hapa. Alikuwa Nuru kwa mmoja, na giza kwa mwingine. Waisraeli, basi, baada ya Musa kuomba, wangeweza kulala kwa amani. Sasa tazama.

> *Musa akaunyosha mkono wake juu ya bahari;* BWANA *akairudisha nyuma bahari kwa upepo wa nguvu wa mashariki usiku kucha; akaifanya bahari kuwa nchi kavu, maji yakagawanyika.*
>
> *Basi wana wa Israeli wakaenda katikati ya bahari katika nchi kavu;. . .*

146 Kama utaangalia, wakati wana wa Israeli, waliokuwa wametoka gizani na kuikubali Nuru, walipopata shida, Nuru iligeuka nyuma. Nao wakalala usiku kucha. Na walipokuwa wamelala, Mungu alikuwa akituma upepo, ukivuma baharini, na kufungua njia ya kutokea.

147 Haleluya kwa Mwana-kondoo! Nina furaha sana kwamba nimejazwa na Roho Mtakatifu, usiku wa leo. Tunapolala, tukifurahia, tukipumzika katika ahadi ya Mungu!

148 Mungu aliwaahidi, kutengeneza njia ya kutoroka. Na walipokuwa wakistarehe juu ya ahadi hii, Mungu alikuwa kule chini, mbele yao, akifungua njia.

149 Kila mwanamume na mwanamke, usiku wa leo, ambaye atamkubali Yesu Kristo katika misingi hiyo; Roho Mtakatifu, wakati umelala, wakati umetulia katika ahadi Yake. Labda wewe ni mlemavu; labda wewe ni kipofu; labda huwezi kusikia; labda huwezi kuona; labda wewe ni mgonjwa; ugonjwa wa moyo, kansa, ama chochote kile, ukifa. Ipokee Nuru, usiku wa leo, na utulie juu Yake.

150 Na upepo, ukija kama upepo wa nguvu ukienda kasi katika Siku ya Pentekoste, utapita huko na kukufungulia njia, haleluya, hata utapita moja kwa moja katika bonde hilo la magonjwa, urudi moja kwa moja kwenye nchi ya afya tena. Utapitia moja kwa moja katika nchi hiyo ya dini baridi, rasmi, zilizotiwa pingu, zisizojali; kwa moyo uliojazwa na Roho Mtakatifu, wenye furaha, wenye shangwe, uliojaa furaha.

151 Mungu anaonyesha nguvu Zake, na alikuwa akizionyesha. Samahani, ninapiga kelele sana. Inaonyesha ukombozi kwa nguvu. Alionyesha damu kule nyuma, juu ya kitu kimoja. Alionyesha nguvu Zake hapa, kwa Damu Yake, kupitia ukombozi. Alionyesha nguvu Zake za kuepuka kifo, kupitia damu. Alionyesha nguvu Zake kufanya njia ya kutorokea, kwa ukombozi wa nguvu.

152 Na, leo, ninyi mliokubali, amina, ninyi mlioikubali Damu ya Yesu Kristo, kukusafisha na dhambi, nguvu za Roho Mtakatifu ziko hapa kukuongoza kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nguvu za Mungu ziko hapa kukubadilisha kutoka kwa ugonjwa hadi afya. Mungu, akisonga mbele, katika kutoka kwa Kanisa Lake! Anaingia kwenye kuchanua, ambapo Mungu atakusanya, baada ya kitambo kidogo, punje Yake. Ajabu, akitoka gizani, kuingia kwenye Nuru ya ajabu! Jinsi tunavyopenda hilo! Jinsi ninavyofanya! Hiyo ina maana gani kwa nafsi yangu, usiku wa leo! Marafiki, nyinyi . . .

153 Nilikuwa nikizungumza na mwanamume mmoja leo, ambaye alikutana nami tu nilipokuwa nje. Naye akasema, "Nimekuwa nikijaribu kuwaambia watu." Kasema, "Nimebadilika sana, Billy, tangu ulipokuwa mtoto." Akasema, "Ulikuwa ukipita na kuniambia, mahali pangu pa biashara, ya kwamba yanipasa kuwa sawa na Mungu, ninapaswa kuwa sawa na Mungu." Na akasema, "Kwa namna fulani nilikucheka. Lakini," kasema, "Billy, mambo yamebadilika sasa." Akasema, "Najua sasa unazungumza nini."

Nikawazia, "Mungu asifiwe!"

154 Akasema, "Ninajaribu kuwaambia wengine juu yake," na kusema, "watabadilisha mada na kuanza kuzungumza juu ya karatasi ya kuchekesha au jambo fulani. Lo, si mimi. Huyu

jamaa anayefuata kwenye kona, anaweza kufa. Yeye ndiye anayefuata. Labda nambari yake ndiyo inayofuata, bila kujua ni nambari ya nani inayofuata." Huenda ikawa ni yako, usiku wa leo, rafiki. Huu unaweza kuwa ndio wakati Mungu anakuita.

155 Mungu, Roho Mtakatifu mkuu, akisimama hapa usiku wa leo, kati ya mauti na Uzima; amesimama hapa usiku wa leo, kati ya ugonjwa na afya. Ninajua ninachozungumzia. Hiyo ni kweli. Sasa hivi, Roho Mtakatifu yule yule unayemhisi sasa, kila mtu aliyezaliwa mara ya pili hana budi kuhisi Roho huyo chumbani. Huwezi kujizuia. Kama una Uhai wowote, unajua upo. Vema.

156 Jinsi ambavyo kama sumaku, wakati ni . . . Wakati sumaku kubwa inakuja karibu na nyenzo, huanza kusonga na kutambaa, (kwa nini?) inakaribia. Kama sumaku kubwa iliyoshuka, juu hapa, wakati mmoja, kule Hammond, Indiana. Nilikuwa nawatazama wakichukua takataka za chuma, sakafuni. Walivuta wenzo mkubwa mno; ikashuka sumaku kubwa mno. Na wakafanya takataka zote za chuma zifagiliwe katikati ya sakafu. Na ilipokuwa ikipita, takataka hizo zote zilivutwa kwenye hiyo sumaku, chuma, zikaenda moja kwa moja na kwenda na sumaku, nje. Nao wakaiondoa sumaku, wakaitupa kwenye kuba, na kuifinyanga tena. Kulikuwa na takataka nyingi za aluminiamu zilizobaki. Nikasema, "Kwa nini hazikuenda?"

Akasema, "Hazina uwezo wa kuvutwa na sumaku."

157 Nikasema, "Mungu asifiwe." Nikasema, "Kwa nini hizi hazikwenda, hapa chini, kipande hiki cha chuma?"

Kasema, "Ukitazama, kimefungwa chini."

158 Na hiyo ni kama watu wengi usiku wa leo, marafiki. Umekuwa mshiriki wa kanisa, lakini hujatiwa sumaku na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kisha unaruhusu kitu fulani kikufunge, tofauti fulani, kikufunge chini.

159 Lakini moja ya siku hizi, kuna sumaku kubwa inayokuja kutoka Mashariki, inayoitwa Mwana wa Mungu, ambayo itafagia nchi hii. Na kila mtu ambaye amekufa katika Kristo atafufuka pamoja Naye, kwenda kule. Na miili hii ya kale itageuzwa na kufanywa kwa sura Yake, kwa mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, ambapo tutaishi milele na milele, bila magonjwa, bila uzee, bila chochote kingine; na katika Utukufu wa Mungu, kuishi katika Uwepo Wake uliobarikiwa milele. Amina. Usiache hilo likutishe. Najisikia kubarikiwa sasa hivi. Hakika ninajisikia. Vema.

160 "Kwa maana ninajua ya kuwa mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya dunia hii; ingawa mabuu wa ngozi wanaharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu; ambaye nitamwona mwenyewe; macho yangu yatamtazama, wala si mwingine."

161 Usifikiri mimi nina wazimu. Sivyo nilivyo. Ikiwa ninao, niache tu. Nina furaha zaidi kwa njia hii kuliko nilivyokuwa kwa njia ile nyingine. Naam, bwana. Acha tu nibaki hivi. Loo, hakika, "wazimu," kwa ulimwengu, kwa kuwa, mambo hayo ambayo ulimwengu unayaita kuwa ya kichaa, Mungu anayaita heri. Huna budi "kupoteza akili yako," kwa ulimwengu huu, kwa sababu (kwa nini?) wewe si wa ulimwengu huu.

162 Unapovuka mstari huo unaotenganisha, unakuwa raia mwenzi wa Ufalme wa Mungu. Loo, jamani! Ni nzuri jinsi gani? Mbona, unakuwa kiumbe kipya, (loo, jamani) umebadilika kutoka hiki ulicho sasa. "Ninyi sasa ni wana wa Mungu. Sasa tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni." Si, "tutakuwa," katika Milenia. Ndivyo tulivyo sasa, sasa hivi sisi ni wana wa Mungu. "Sasa hivi tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni, katika Kristo Yesu," sio tu kanisani, "katika Kristo Yesu."

163 Bwana Yesu aliyefufuka yuko hapa. Yuko hapa katika nguvu Zake. Yuko hapa katika nguvu Zake za ukombozi. Yuko hapa kwa ajili ya kutoka. Yuko hapa kuleta kila mshiriki wa kanisa katika ushirika na Yeye. Yuko hapa kuleta kila mwenye dhambi, haijalishi uko chini kiasi gani, Yuko hapa kuleta nguvu za kufufuka Kwake katika maisha yako na kukufanya kiumbe kipya.

164 Hapa, miaka michache iliyopita, dini zote za ulimwengu zilikutana, ninaamini ilikuwa London, Uingereza, ama mahali fulani. Sikumbuki haswa. Lakini, wakati wote walipokuwa wakizungumza kwa ajili ya makanisa mbalimbali, Waislamu, na wa Buddha, na kila kitu. Maskini. . . jamaa aliyewakilisha kanisa la Utakatifu la Marekani, John Witt, naamini, lilikuwa jina lake. Kwa hiyo basi alipoinuka, wakati wake wa kunena, dini zote ziliwakilishwa katika kusanyiko hili kuu, alisimulia hadithi ya Lady Maccabee, jinsi alivyokuwa duni; alikamatwa huko Oklahoma, akiwa na sigara kinywani mwake, akiendesha gari a. . . au kuvunja sheria ya mwendo kasi, kupita mitaani na gari la abiria. Alikuwa amefanya mauaji mengi sana, na ni mchafu sana, na mbaya sana, mpaka, walipoenda kumwadhibu kwa kumpaka lami na kumpamba manyoya, hata wasingeweza kuweka mikono yao juu yake, wakiogopa kwamba wangechafuka.

165 Na alipoisimulia hadithi hiyo kwa njia ya mchezo hivi kwamba, hata kila msikilizaji alikuwa ameketi kwenye ncha za viti vyao. Alisema, "Waungwana, wa dini za ulimwengu huu, dini yako ina chochote ambacho kingesafisha mikono ya Lady Maccabee?" Hakuna aliyesema neno. Aliruka juu hewani na kupiga visigino vyake pamoja, na kupiga mikono yake. Akasema, "Damu ya Yesu Kristo haitasafisha mikono yake tu, bali itausafisha moyo wake." Amina. Hiyo ni kweli.

166 Damu ya Yesu Kristo itamchukua kahaba wa chini kabisa huko Louisville, Kentucky, na kufanya mwanamke wa heshima, mtakatifu kutoka kwake. Itamtoa muuzaji pombe haramu kutoka mahali hapo chini, na kufanya mtu muungwana kutoka kwake, na mtakatifu wa Mungu.

167 Rafiki zangu, raia wa Ufalme, wanaume wenzangu wa Kentucky na Indiana, na karibu! Je, hamfikirii, usiku wa leo, ni wakati wenu kumtafakari huyu Bwana Yesu, kabla nafasi yako ya mwisho haijachukuliwa?

168 Wakati, unaona Kanisa likienda katika msafara huu mkuu, unaona ile Nguzo ya Moto ikitangulia mbele yetu; wakisimama, wakifanya miujiza na ishara. Yuko hapa, usiku wa leo, katika nguvu Zake zote za ukombozi. Yeye yuko hapa kumponya, kila mwenye dhambi, kumrejesha kila aliyerudi nyuma. Yuko hapa kumponya kila mgonjwa.

169 Yeye ndiye Injili yote. Nasi tunahubiri Injili yote; kula Mwanakondoo mzima. Umchome kwa Roho Mtakatifu, na ujue ya kwamba ni mlo mzuri, kwa maana Roho Mtakatifu ametujulisha kiungu kwamba ni mzuri kweli kweli. "Onjeni muone, Bwana ni mwema. Ina ladha ya asali kwenye mwamba."

170 Bwana wetu Yesu hapa, katika upendo na nguvu Zake, katika baraka Zake kuu za ukombozi! Loo, jinsi anavyosimama kati ya kanisa na dhambi, usiku wa leo! Jinsi anavyosimama kati yenu na hukumu; akitokwa damu, akiomba!

171 Hapa si muda mrefu uliopita, nilienda mahali fulani hapa Ohio, ambapo nilikuwa karibu kutoa maoni yangu juu ya hukumu. Nilikuwa nikila kwenye mkahawa mdogo wa Dunkard. Tulikuwa na mkutano mzuri. Ilinibidi kukaa maili kadhaa nje huko bara, kwenye moteli ndogo. Nilikuwa nikila kwenye mkahawa wa Dunkard; watu wazuri, na Jumapili walifunga na kwenda kanisani. Ilinibidi kuvuka hadi maskini mahali duni, pa kawaida, pa Marekani kula chakula changu cha jioni.

172 Nilipoingia mlangoni, kwa mshangao wangu, hapo alisimama polisi wa serikali akiwa amemkumbatia msichana kwa mikono yake, akicheza mashine ya kupangwa. Sasa, kucheza kamari ni haramu katika Ohio, na hapo mtu wa sheria mwenyewe anavunja sheria. Na pengine, mwanamume katika umri wangu, labda aliyeoa, mwenye familia mahali fulani; huku akiwa amemkumbatia msichana fulani aliyesimama pale.

173 Nilitazama nyuma kwenye mgahawa, wavulana wengine wameketi kule nyuma, wamelewa, na msichana akitenda bila uadilifu hata kidogo. Nilitazama, nikikaa chini, upande wangu wa kulia hapa, kwenye kibanda. Ambayo, nilikuwa tayari kuketi.

174 Hapo ameketi bikizee, yapata umri wa miaka hamsini na minane, sitini, rika ya mama yangu; ameketi pale, ngozi ikiwa imekunjamana, amevaa nguo ndogo. Na, loo, ilikuwa ya

kutisha mno. Na kucha zake za miguu zimepakwa zambarau, midomo yake imepakwa zambarau, mwonekano wa kuogofya sana uliowahi kuona. Nywele zake zimekatwa fupi sana na zimejikunja namna *hiyo*. Naye alikuwa akinywa.

175 Hapo wameketi wanaume wawili pamoja naye, wameketi pale, wenye sura ya kutisha, wamelewa, na mmoja wao akiwa amelala kwenye mabamba ya meza. Na walipoomba radhi, wakatoka kwenda msalani . . .

176 Nilisimama hapo. Nikawazia, "Ee Mungu, unawezaje Wewe kuvumilia hili? Unawezaje Wewe kuangalia kama hilo? Wakati, hata moyoni mwangu, na mimi ni mbaya kama nilivyo mimi, hata hivyo, bado sijui kama Sarah wangu mdogo na Rebekah itabidi walelewe katika kizazi kama hiki kuona jambo hilo likitokea. Bwana, kwa nini usiifutilie tu kutoka kwenye uso wa dunia?" Nikawazia, "Kwa nini usifanye hivyo, Bwana?"

177 Nikakaa pale chini na kuanza kulia tu. Nikaona ono. Niliona, tuseme, ulimwengu ukizunguka-zunguka angani, na upinde wa mvua ukasimama kuzunguka ulimwengu huo. Na mtu fulani aliyekuwa akizungumza nami, akasema, "Hiyo ni Damu ya Yesu Kristo, iliyoizunguka dunia hii, ambayo humzuia asiiharibu. Ikiwa Mungu anaweza kuona dhambi, 'Siku utakapokula, siku hiyo utakufa.' Kila mtu chini ya hiyo Damu pale, anayo . . . ana uhuru wa kujiamulia, kuchukua chaguo lako. Lakini kama ukifa, na roho yako ikaruka kupita rehema ya hiyo Damu, tayari umehukumiwa kabla ya kufika huko. Hakuna kilichobakia kwako."

178 Kisha nikajiona mwenyewe. Nilimwona Bwana wangu Yesu amesimama pale, akiwa na taji ya miiba kichwani Mwake, na machozi yakitiririka, yamechanganyikana na damu, yalipokuwa yakilowesha ndevu Zake. Nami nikaona dhambi zangu zikija mbele Zake, na kila wakati zingekuja mbele Zake namna hiyo, [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . mpaka Yeye alikuwa anatetemeka. Miiba ingenata kwenye paji la uso Wake, zaidi. Angeyumbayumba kurudi nyuma. Angesema, "Baba, msamehe, hajui analofanya." Na tena ningefanya jambo fulani, halafu Damu Yake ilikuwa kama bamba kwenye gari, ikilinda gari, kunikinga na ghadhabu ya Mungu, nisivyostahili.

179 Nami nikaja Kwake, polepole, nikampigia magoti. Nikasema . . . Nilitazama kule chini, mbele yangu, na hapo kulikuwa na kitabu cha kale cha dhambi, na jina langu limeandikwa juu yake. Nikasema, "Bwana, utanisamehe?"

180 "Hakika," Yeye alisema, kwa macho ya upendo; akatia mkono ubavuni Mwake, akatoa Damu, na kuandika juu yake, "Umesamehewa." Na kukitupa tena kwenye Bahari ya Usahaulifu. Akasema, "Sasa . . . "

Nikasema, "Asante, Bwana."

181 Akasema, “Sasa, nakusamehe; nawe unamhukumu.” Loo, hiyo ilibadilisha picha, kwangu.

182 Ni—ninatoka kwenye hilo. Nikaenda pale na kukaa karibu naye, na kuanza kuzungumza. Na alikuwa na maisha magumu nyuma kabla yake. Nikasema, “Hivi hukuwahi kuwa Mkristo?”

Akasema, “Nililelewa katika nyumba ya Kikristo.”

Nami nikasema, “Kulifanyika nini?”

183 Akaniambia kuhusu kosa na mume wake, na jinsi watoto, na kadhalika. Nikasema, “Yote, kwa miaka hii yote, hujawahi kuishi kwa amani tangu ulipokutana na Mungu?”

Akasema, “Bwana, huo ndio ukweli.”

Nikasema, “Hivi hutampokea sasa hivi?”

Akasema, “Je, atanichukua?”

Nikasema, “Anabisha moyoni mwako sasa.”

184 Na kutoka kwenye kile kibanda, hapo sakafuni, na kupiga magoti mbele ya hadhara hiyo ya watu; mashine za kamari zilisimamishwa, laana chafu zikakoma, na kila kitu kingine. Nami nikainua mikono yangu, na mikono yangu . . . na maskini mikono hiyo iliyokunjamana, na kumwongoza kwa Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Ni hayo tu, marafiki. Usiangalie . . . Yesu . . .

185 Sijali umefanya nini, dhambi zako ni nyeusi kiasi gani, jinsi maisha yako yalivyo machafu; Mungu amesimama, usiku wa leo, akibisha kwenye mlango wa moyo wako, ili akusamehe, haijalishi wewe ni nani.

186 Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Dada, njoo kwenye piano pale, tafadhali?

187 Baba wa Mbinguni, loo, ninaomba ya kwamba Wewe sasa hivi . . . wakati Roho Mtakatifu anatembea ndani ya jengo hilo. Hebu na tutafute kwanza Ufalme, tupate kibali Kwako, ndipo ninaamini Wewe utawaponya wagonjwa. Lakini sasa hivi, Baba, huku nikihisi kwamba kuna shauku kubwa, ya kina na usadikisho, watu tukijua ya kwamba Kanisa Lako liko katika huko kutoka, nasi tunaendelea kuelekea Hukumuni. Bila kujua lakini, asubuhi, mtu anaweza kuja kando ya kitanda, na hapo tumelala, tumeondoka. Wakati huu, kesho usiku, huenda tukawa katika chumba cha kuhifadhia maiti mahali fulani, na nafsi zetu huko katika Umilele.

188 Ee Mungu, hii inaweza kuwa ndiyo saa ya mwisho! Hii inaweza kuwa ndiyo nafasi ya mwisho ambayo mwanadamu atapata. Wengi, bila shaka, wameketi hapa, wanaume na wanawake, ambao walitamani, ambao wameishi maisha mazuri ya kawaida tu, lakini hawajawahi kuzaliwa mara ya pili, hawajui maana ya kujazwa na Roho Mtakatifu, maisha yaliyosalimishwa kikamilifu; huku minyororo yote, aibu,

ikiondolewa kwao, na Roho wa Mungu awabatize katika rehema Yake.

189 Baba, Mpendwa, hivi Wewe, usiku wa leo, katika Jina la Mtoto Wako mpendwa, Yesu, hutaingia kwenye kila moyo na kusema sasa hivi? Pia wajalie, katika unyenyekevu wa mioyo yao, wakuinulie Wewe mawazo yao, wainue moyo wao na kusema, "Mimi hapa, Yesu. Nichukue sasa, jinsi nilivyo, na unifinyange na unifanye kitu tofauti. Nifanye niwe mtu wa aina ile ungetaka niwe. Katika maisha yangu yote, Wewe umezungumza nami. Umezungumza nami. Umejaribu kunifanya nifanye tofauti. Umejaribu kunifanya nijisalimishe. Lakini sasa siku imeenda sana, Bwana, pamoja nami, lakini niko tayari kuja sasa." Tujalie, Baba. Huku rehema ikiita, kabla ya Hukumu; msafara wa Kanisa, unaondoka Misri; na waje, waende pamoja na kundi kubwa, walioitwa watoke. Tunaomba katika Jina Lake.

190 Na huku tumeinamisha vichwa vyetu, na macho yamefumbwa, na Wakristo wakiomba. Sijui kama ungeinua tu mkono wako, useme, "Ndugu Branham, unikumbuke. Ni—ninaamini kila neno unalosema ni Kweli kuhusu Yesu Kristo. Na sisi sote tunahitaji kujazwa na Roho, na, mimi sijajazwa, bado. Nimekuwa mshiriki wa kanisa." Au, labda hujawa, hata kidogo. Labda umekuwa mwenye dhambi, hujawahi kumkubali Kristo. Au, umekuwa mshiriki wa kanisa, na hujazaliwa mara ya pili. Tafadhali inua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi yako. Nataka kuwa sawa."

191 Mungu akubariki. Mungu akubariki, na wewe, na wewe, wewe, wewe; na wewe, ndugu yangu; na wewe, dada; na wewe, ndugu; wewe, wewe, wewe, ndugu, dada. Naona.

192 Loo, upande wangu wa kushoto, ni wangapi hapa? Inua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham, ninataka kuzaliwa."

193 Sasa, kumbuka, Roho Mtakatifu anazungumza na wewe. Ikiwa mimi ni mtumishi wa Mungu, najua, hakika kama ninavyosimama kwenye jukwaa hili, kwamba Roho Mtakatifu anazungumza na mioyo hapa. Marafiki, ninaweza kuwa mtu wa kipekee kwenu, lakini mimi si mshupavu. Najua ninachozungumzia; ikiwa najua shida yako ni nini huko nje, na ugonjwa wako ni nini, na Mungu anasikia maombi yangu kwa ajili yako. Na papa hapa katika jengo hili wameketi watu ambao wameponywa, wakiwa na kansa, na upofu, na uziwi, na vilema, na chochote kile. Angalia mikutano duniani kote. Vipi kuhusu wewe sasa? Vipi kuhusu hilo sasa? Kama atasikia maombi yangu kwa ajili ya hilo, je, hatasikia maombi yangu kwa ajili ya hali yako ya nafsi yako? Kama atanifunulia shida yako ilipo, je, hatanifunulia sasa ilipo shida yako, pia?

194 Ni wangapi zaidi watainua mkono wako, useme, "Ndugu Branham nikumbuke. Nataka, kwenye wakati huu, nimwombe

Mungu anirehemu"? Mungu akubariki, na wewe, na wewe, wewe, tena. Loo, jamani, kote tu jengoni, kila mahali!

195 Huku mmeinamisha vichwa vyenu. Sijui kama wewe, uliyeinua mkono wako, uwe na neema zaidi kidogo tu, useme, "Bwana, nilikuwa na neema ya kutosha kuinua mkono wangu, nipe neema ya kutosha kusimama wakati anapoomba. Kama atakuja kunichukua, kabla ya mapambazuko, Bwana, hii ndiyo ishara yangu Kwako, ya kwamba ninataka kuwa sawa. Ninataka kukutana na Wewe siku moja. Kikohozi hiki kitaninyemelea na nitabonyeza foronya ya kifo. Daktari ataondoka kando ya kitanda changu; hakuna kitu kingeweza kufanywa. Basi, Mungu, irehemu nafsi yangu. Wakati ukungu baridi wa mauti unaelea mle chumbani, jalia meli ya zamani ya Sayuni ije, inibebe. Nitasimama, Bwana. Inachukua neema nyingi, lakini Kitu fulani kinanisogeza. Nimesimama." Mungu akubariki, ndugu.

196 Mtu mwingine atasimama, aseme, "Ninasimama, Bwana." Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu, dada. Baki tu umesimama. Kila mtu ambaye anataka kukumbukwa katika maombi haya, kwa wokovu wa roho yako, naomba usimame. Mungu akubariki. Mungu akubariki, kijana. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada yangu. Mungu akubariki, dada; wewe, ndugu.

197 Mtu mwingine simama sasa na kusema, "Niko hapa. Ndugu Branham, sijasimama mbele yako. Ninasimama mbele za Mungu. Kitu fulani kiliniambia nisimame, nami nimesimama." Je, utafanya hivyo? Simama tu kwa miguu yako. Mchukulie tu Mungu kiasi hiki. Mungu akubariki, mama.

198 Kuna wengine. Mungu akubariki, mama. Hiyo ni sawa. Maskini mama akiwa amemshika mtoto wake mdogo akijaribu kunyanyuka, machozi machoni mwake. Hivi hutakuja? Simama tena. Mungu akubariki, mama, bikizee alisimama pale, na mkongwe kwelikweli, akijua ya kwamba hana budi kumkabili Mungu, moja ya siku hizi. Mungu akubariki. Nani mwingine atasimama sasa, aseme, "Nitasimama"?

Baki tu umesimama kwa ajili ya maombi.

199 Mtu mwingine? Ninahisi tu kama kuna mtu mwingine anayetaka kusimama. Labda unataka tu kuja karibu zaidi kidogo. Usiiahirishe tena. Simama tu. Je, utafanya hivyo? Ninyi mnaotaka kuwa karibu na Mungu. Mungu akubariki. Hiyo ni sawa. Je, mtu . . . Mungu akubariki, mama. Ndiyo, bwana.

200 Kuna angalau watu watatu zaidi, ninaowatazama moja kwa moja, wanaopaswa kusimama, maana huyo hapo amesimama Malaika wa Mungu. Mungu akubariki, mama. Hiyo ni kweli. Sasa, vema, ndugu, vipi kuhusu hilo? Vema. Na, Malaika wa Bwana akisimama, najua. Ninamwona, nami ninajua ya kwamba mtu fulani anapaswa kusimama sasa hivi. Nitasubiri dakika moja zaidi. Mungu na . . . Unajua Yeye anasukuma

moyoni mwako. Amesimama hapo, rafiki yangu. Huyo ndiye anayekuambia simama. Hivi hutafanya hivyo? Simama tu na umkubali, sasa hivi. Vema.

201 Una uhakika sasa? Kama Mungu angekuita usiku wa leo, katika mkutano huu; mahubiri haya, mwaliko huu, yatakutana nawe kule utakapokufa. Umefanya nini kuhusu hilo? Kama huna hakika, kweli, simama sasa, kusudi Yeye aone unataka kukubali, kutembea katika Nuru.

202 Sasa, Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, hawa watoto Wako wapendwa, mioyo iliyolainishwa, Neno lilianguka moyoni mwao usiku wa leo. "Imani huja kwa kusikia, na kusikia Neno." Na Wewe ungeweza kusikia. Na Wewe ulilainisha mioyo yao, wengi wamesimama, wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, wanakukiri Wewe kama Mwokozi na Kiongozi wao mpendwa.

203 Pia jalia Malaika wa Mungu, Yule aliye hapa sasa usiku wa leo, na awaongoze maishani. Jalia waongozwe hadi Kalvari sasa hivi, mioyoni mwao, na wamkubali Yesu kama Mwokozi wao. Tena jalia Roho Mtakatifu, kwa Damu ya Kristo, ashuke juu ya nafsi zao, na kuondolea mbali kutokujali kwote, na kuwajaza kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Jalia huu uwe usiku mkuu zaidi wa maisha yao. Tunajua ndivyo ulivyo, kwa maana usiku wa leo wanakupokea Wewe. Tujalie, Bwana, sasa hivi. Basi jalia waende nyumbani kutoka hapa, usiku wa leo, wakiwa na furaha na wakishangilia, wakimsifu Mungu, kwa moyo wao wote. Ninaomba baraka hii kupitia Jina la Yesu Kristo.

Sasa Bwana awabariki mnapoketi.

204 Hebu niwaulize sasa. Kila mmoja wenu aliyesimama, na unajua ya kwamba jambo fulani limefanyika kwako ulipokuwa umesimama, inua mkono wako. Inua tu mkono wako, unajua jambo fulani limetukia. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Inabidi, marafiki. Inabidi. Nilisimama, nimeona hapa sasa hivi, Malaika yule yule ninayenena habari zake, akipitia moja kwa moja kwenye jengo hili hapa; Malaika yule yule wa Bwana, ile Nguzo ya Moto. Nimekuwa nikihubiri dakika tano ama kumi zilizopita, chini ya uvuvio huo. Ninaihisi, ninaiona tu ikipita kwenye jengo hili. Sasa, mnaweza kufikiri ya kwamba ninawasimulia hadithi, lakini ni Kweli.

205 Sasa, hata sidhani nitaita mstari wa maombi. Nafikiri nitasimama papa hapa na kumwomba tu Mungu athibitishe ya kwamba nimewaambia Kweli, hiyo ni kweli, kwa ishara, maajabu.

206 Ni wangapi hapa ndani wanaotaka kuponywa, watu wagonjwa? Inueni mikono yenu, popote ulipo. Inua tu mkono wako, useme, "Ninaikubali." Vema.

207 Nataka utazame, uishi, na uamini. Mtu fulani katika kusanyiko hili, kupitia *hapa,* mtu kupitia hapa, angalia tu, na kusema, "Bwana Yesu . . ."

208 Hivi. Ninaamini, sababu ya kufanya wito huo wa madhabahuni kwanza, hatuna budi kupata kibali Kwake. Hili ni jambo jipya kwangu. Sina budi kupata kibali Kwake, kwanza. Basi ikiwa nimepata kibali, na kufanya fadhili . . . Nanyi, kumi na mbili, au mbili, nafsi zinamjia Yeye wakati huo huo. Hakika, hakika . . .

209 Sasa ninyi, kila mmoja wenu ninyi watu mnaomjia Kristo, basi, tafuta kanisa zuri lililojazwa na Roho Mtakatifu na uende huko. Na hapo utafute ubatizo Wake mpaka uupate; nenda tu, kila usiku tu, kila siku, endelea tu kuomba. Na wakati unatafuta . . .

210 Sasa, ninyi watu ambao ni wagonjwa. Kama nimewaambia Kweli, Mungu atashuhudia ya kwamba ni Kweli. Hiyo ni kweli. Inaweza tu kuifanya. Na Mungu atalijulisha, kama utaomba tu na kuamini kwa moyo wako wote. Angalia tu, na useme hivi . . .

211 Wakati Malaika wa Bwana alipokutana nami kule Green's Mill, Indiana, miaka minane iliyopita; baada ya kuwa tangu utotoni, akinifuata, akionyesha maono. Nilipomwendea, alisema, "Kama utakuwa mwaminifu, wafanye watu wakuamini, hakuna kitakachosimama mbele ya maombi."

212 Sasa, Yeye angeweza kukufanyia vivyo hivyo sasa yale aliyoweza wakati ule. Amefufuka kutoka kwa wafu. Na Yeye . . . hapo kusanyiko huko nje mbele Zake. Anajua yaliyo juu ya kila mmoja wenu, yale ambayo umefanya, shida yako ni nini, kila kitu kuhusu hilo. Je, unaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi iamini kwa moyo wako wote.

213 Ninaona kijana aliyeketi hapa, akiamini, akijaribu, akiwa na imani. Je, unaamini kwamba Mungu atanijulisha tatizo lako? Unaamini? Kama akinijulisha, je, utakubali uponyaji wako? Una shida ya moyo. Hiyo si ni kweli? Vipi kama ningekuambia sasa kwamba ulipona huo? Je, ungeamini? Simama kwa dakika moja. Una moyo wenye wasiwasi, na moyo wa kunung'unika. Imekusumbua kwa muda. Wakati pekee, unapolala, pia, unakusonga, na unapiga sana huku na huko, ukipepea. Je, hiyo ni kweli? Maana, husababisha kutokumeng'enya chakula kutoka kwa tumbo lako, kuja kupitia kwenye mshipa huo. Hiyo si ni kweli? Hutasumbuliwa nao tena. Weka tu ulicho nacho sasa hivi; unaweza kwenda nyumbani na uwe mzima.

214 Sisomi mawazo yako. Mimi ni mgeni kabisa kwako. Wewe ni mwanaume tu uliyeketi hapo. Je, hiyo ni kweli? Sijawahi kukuona maishani mwangu, na sikujua lolote kukuhusu. Je, hiyo ni kweli? Amini kwamba Bwana yuko hapa!

215 Kusema kweli, kijana, nataka kukuuliza jambo fulani, nawe uone kama hii ni kweli au la. Yapata dakika chache tu zilizopita, kwa ghafula, kitu cha kigeni kilikuja juu yako nilipoanza kuzungumza kuhusu "uchungu umetoka kwenye mwiba." Hiyo si ni kweli? Hivi haikuwa hisia ya ajabu uliyokuwa nayo, ukiwa umeketi hapo? Hiyo si ni kweli? Na si ulinitazama wakati huo huo, na macho yangu yakakupata wakati huo huo? Hapo ndipo ulipoponywa, na ugonjwa wa moyo, papo hapo. Amina. Hiyo ndiyo hasa. Yuko hapa.

216 Sisomi mawazo yenu, marafiki. Ninasema tu Kweli, na Mungu huithibitisha kuwa ni Kweli.

217 Unafikiri nini kuhusu hilo, uliyeketi hapo karibu naye? Unaamini? Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Je, unaamini kama Mungu... Uliyeketi mbele, hapa kwenye kiti cha mbele, hiyo ndiyo sababu ninazungumza nanyi sana, Roho kule nyuma kule, kunizunguka. Lakini unaamini, nikiweza kuwasiliana na roho yako, Mungu atafunua kilicho shida yako? Je, utakubali uponyaji wako? Wewe ni mgonjwa wa kisukari. Je, hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Simama kwa miguu yako. Je, unakubali uponyaji wako sasa? Bwana Yesu Kristo na akufanye uwe mzima kabisa. Mungu akubariki.

218 Kuwa na imani. Mtu fulani *hapa* ndani anaamini. Kuwa na imani, kwa moyo wako wote.

219 Ninamwona kijana ameketi hapo amevaa suti ya bluu. Hiyo hapo imesimama moja kwa moja juu yake. Una ugonjwa wa ngozi, sivyo, kijana? Hiyo si ni kweli? Simama kwa miguu yako. Loo, naona, uko pamoja na wajumbe hawa. Je, hiyo ni kweli? Vema, unataka kwenda nyumbani ukiwa mzima? Inua mkono wako na useme, "Bwana Yesu, sasa naamini Malaika wa Bwana anaongoza. Nami ninaamini kwamba nimepona."

220 Unafikiri nini juu yake, mtu wa pili kutoka kwake hapo, unaamini, pia? Simama kwa miguu yako kwa dakika moja, ili niweze kukutazama. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu; kwa moyo wako wote? Je, unataka kuishinda shida hiyo ya moyo? Hiyo ndiyo uliyokuwa nayo, sivyo? Hiyo ndiyo wewe "*ulikuwa nayo*," nikasema. Hunayo sasa. Unaweza kwenda nyumbani, pia.

221 Mtu anayefuata baada yake, una maoni gani juu yake, bwana? Je, unaamini kwa moyo wako wote? Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Simama kwa miguu yako. Je, unaamini kwa moyo wako wote sasa? Ulikuwa na wasiwasi. Hiyo si ni kweli? Unaona? Je, hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Unaweza kwenda nyumbani mzima sasa. Yesu Kristo akuponya.

222 Vipi kuhusu mtu anayefuata, simama, chini kwenye safu, unaamini kwa moyo wako wote? Simama kwa miguu yako. Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini Yeye angeniambia una shida gani,

kwamba ungekubali uponyaji wako? Iko kwenye koo lako. Je, hiyo ni kweli? Nenda nyumbani ukawe mzima, katika Jina la Yesu Kristo.

223 Mtu mwingine yeyote katika jengo hili, anayetaka kuponywa, anaweza kusimama na kuponywa. Ikiwa umeniamini mimi, kama mtumishi wa Mungu, simama kwa miguu yako. Mungu akubariki. Shida ya kike, kansa, hiyo hapo inaondoka. Mungu abarikiwe! Kila mmoja wenu, inueni mikono yenu kwa Mungu.

224 Baba yetu wa Mbinguni, sasa ninalaani kila ugonjwa wa jengo hili, ninafukuza kila pepo mchafu, na Roho Mtakatifu atawale sasa na kumfanya kila mtu kuwa mzima.

225 Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, na kusema, “Bwana asifiwe,” kila mahali. Basi shangilieni na muwe na furaha, kwa maana Yesu Kristo yuko hapa, Mwana-Kondoo wa Mungu, kuwaponya ninyi, kila mmoja.

*UKOMBOZI KWA NGUVU* SWA54-0329
(Redemption By Power)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumatatu jioni, tarehe 29, Machi, 1954, katika Kanisa La Mlango Uliofunguliwa huko Louisville, Kentucky, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org